Kisima cha Zamzam ni nini, na ukweli wake ni upi?

---

Angalizo: Makala hii haina lengo la kushambulia Imani Fulani, wala kushabikia Imani Fulani, pia haina lengo la kumchafua mtu yoyote, wala kumdhalilisha, bali kutoa elimu sahihi kuhusiana na tunayoamini na yanayoaminiwa.

---

Kisima cha “Zamzam”, ni kisima kilichopo katika msikiti wa Al Haram uliopo Makka, katika nchi ya Saudi Arabia. Kisima hiki kipo umbali mfupi kutoka katika jiwe/jabali jeusi la Kaaba. *(umbali wa mita 20 mashariki mwa jiwe hilo).*

Kulingana na Uislamu, kisima hiko kilijitokeza hapo kimiujiza kipindi kile Hajiri kijakazi wa Sara alipoachwa na Abramu katika lile jangwa *(katika vilima vya Safa na Marwah)* na akakosa maji ya kunywa yeye na mwanae Ismaili.

Na Hajiri alipoona mwanae anakaribia kufa, akaanza kuzunguka vilima hivyo vya Safa na Marwah mara saba, na alipokuwa katika mzunguko wa saba, ndipo Malaika Jibra’il *(Gabrieli)* akatokea na

kukitokeza kisima hiko kimiujiza na kilipotokea, Hajiri akaanza kusema zamzam, maana yake “acha kutiririka”

Hadithi za kiislamu zinazidi kusema kuwa kisima hiko kilikauka, lakini kikaja kuvumbuliwa tena na babu yake Muhamad aliyeitwa Muttalib katika karne ya sita(6).

Lakini pia binamu yake Muhamad aliyeitwa “Ibn Abbas” alisema *“Maji ya zamzam yanafaa kwa nia yoyote ile, mtu akinywa kwa lengo la kupona ugonjwa basi mungu atamponyesha kupita maji hayo, kama mtu atakunywa kwa lengo la kuondoa njaa, basi mungu ataiondoa njaa yake, kama mtu atayanywa kwa lengo la kukata kiu basi mungu ataikata kiu yake kwasababu hata Ismail alikunywa maji hayo na kukata kiu yake kali”*.

Na kwasababu hiyo maelfu ya watu wanayatumia maji hayo wakiamini yamebeba uponyaji wa kimungu ndani yake??. (Je ukweli wa mambo haya ni upi)?

Awali ya yote tufahamu kuwa Ishamaeli, mwana wa Hajiri hakuwa mwana wa Ahadi kulingana na biblia, hali ISAKA, mwana wa Sara ndiye aliyekuwa mwana wa Ahadi.  Hadithi zote zilizopo na zinazotungwa zinazoshinikiza kuwa Ishamaeli ndiye mwana wa

Ahadi, si za kweli.

Ishmaeli aliahidiwa Baraka nyingine za Mungu lakini si za Mzaliwa wa kwanza. Baraka za mzaliwa wa kwanza zilikuwa kwa Isaka aliyekuwa mwana wa Sara.

Sasa ukweli wa kisima hiko kibiblia ni upi na je kuna muujiza wowote katika kisima hiko?

Habari ya kisima hiko, ambako biblia haisemi kwamba kinaitwa “Zamzam” inapatikana katika kitabu kile cha Mwanzo 21, Hebu tuianzie ile habari mbali kidogo katika ule mstari wa 9 ili tuielewe habari..

> *Mwanzo 21:9 “Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka.*
>
> *10 Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka.*
>
> *11 Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa*

*ajili ya mwanawe.*

*12 Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa.*

*13 Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyu naye ni uzao wako.*

*14 Ibrahimu akaamka asubuhi na mapema akatwaa mkate na kiriba cha maji, akampa Hajiri akimtwika begani pake, na kijana, akamruhusu; naye akatoka, akapotea katika jangwa la Beer-sheba.*

*15 Yale maji yakaisha katika kiriba, akamlaza kijana chini ya kijiti kimoja.*

*16 akaenda akakaa akimkabili, mbali naye kadiri ya mtupo wa mshale; maana alisema, nisimwone kijana akifa; naye akakaa akimkabili, akapaza sauti yake, akalia.*

*17 MUNGU AKASIKIA SAUTI YA KIJANA. MALAIKA WA MUNGU AKAMWITA HAJIRI KUTOKA MBINGUNI, AKAMWAMBIA, UNA NINI, HAJIRI? USIOGOPE, MAANA MUNGU AMESIKIA SAUTI YA*

> *KIJANA HUKO ALIKO.*
>
> *18 ONDOKA, UKAMWINUE KIJANA, UKAMSHIKE MKONONI MWAKO, KWA KUWA NITAMFANYA KUWA TAIFA KUBWA.*
>
> *19 mungu akamfumbua macho, naye akaona kisima cha maji; akaenda akakijaza kiriba maji, akamnywesha kijana.*
>
> *20 mungu akawa pamoja na huyo kijana, naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde.*
>
> *21 akakaa katika jangwa la parani; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya misri".*

Sasa kulingana na maandiko hayo matakatifu, ni Dhahiri kuwa Ishmaeli (au Ismail), hakuwa mwana wa ahadi ndio maana aliondolewa katika hema ya Sara, na Mungu alikuwa upande wa Sara. Lakini kwasababu Mungu ni wa rehema asingeweza kumwacha kabisa Hajiri na Ishamaeli kwani nao pia ni uzao wa Ibrahimu, ndio maana akawaokoa na mauti katika jangwa lile lisilo na maji.

Na utaona Malaika wa Mungu alimfumbua macho Hajiri ili akione kisima, na si kwa *“alikitokeza kisima kile kimiujiza”*.. Maana yake ni kwamba kisima kile tayari kilikuwepo pale, isipokuwa macho ya Hajiri hayakukiona, na yalipofumbuliwa ndipo akakiona na kumshukuru Mungu.

Sasa swali la Msingi ni hili, je kisima hiko kiliendelea kuwepo?, na je Mungu aliagiza chochote juu ya kisima hiko, kwamba watu waende huko kuchota maji yake?

Jibu ni kwamba kisima hiko kiliendelea kuwepo, kwasababu kilikuwepo kabla ya hapo pia!..na ulipofika wakati kilipotea kama tu visima vingine vilivyopotea… Na wala maji yake hayakuwa na muujiza wowote kwa Ishmaeli Zaidi ya maji mengine yoyote.

Yale yalikuwa ni maji ya kawaida tu, ambayo mtu akinywa anakata kiu, na ndilo lililokuwa lengo la Mungu, kwa Hajiri na Ishmaeli, kwamba wanywe wakate kiu basi, waweze kuokoka na mauti ya kukosa maji, na si kwamba wakifanye kuwa kisima kitakatifu cha kufanyia ibada.

Sasa kulingana na hadithi za kiislamu, wanakiri kuwa kilipotea hiko kisima, lakini ajabu ni kwamba kimekuja kugunduliwa na

kufukuliwa karne ya 6, *(Jambo hilo si kweli, ni uongo wa adui).*

Huenda hiko kisima kilichopo sasahivi ni kisima tu kilichoibuliwa na watu, na zaidi hata kama kingekuwa ni chenyewe (halisi) kile alichoonyeshwa Hajiri na Malaika, kisingekuwa na Uungu wowote ndani yake kwani Mungu hajawahi kuweka agano lake katika visima! Au mito au bahari.

Ingekuwa ndivyo basi ule mto Yordani ambao Naamani-Mkoma aliokwenda kuoga mara saba na ukoma wake kuondoka basi hata leo wakoma na wagonjwa wangetiririka pale kuoga ili kupona magonjwa yao…

> *2Wafalme 5:9 "Basi Naamani akaja na farasi wake na magari yake, akasimama mlangoni pa nyumba ya Elisha.*
>
> *10 Naye Elisha akampelekea mjumbe, akisema, Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi………………*
>
> *14 Ndipo akashuka, akajichovya mara saba katika Yordani, sawasawa na neno lake yule mtu wa Mungu; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto*

> *mchanga, akawa safi".*

Sasa huo ni mto Yordani ambao mpaka leo upo! Na ndio mto Bwana YESU aliobatizwa na Mbingu zikafunuka juu yake kumshuhudia.. Lakini maji yake leo hayawezi kutumika kama maji ya kiungu.. Vipi hayo mengine?.

Na pia kisima hiko cha Hajiri hakikuwepo Saudi Arabia, bali kilikuwepo Parani katika jangwa la Sinai.

Kwahiyo maji hayo ya zamzam, yanayotoka huko Saudi Arabia, *(Makka)*, si maji ya kiungu na  mkristo/asiye mkristo hapaswi kuyatumia kwa matumizi yoyote, matokeo ya kutumia maji hayo kwa lengo la kupata uponyaji, au utatuzi wa tatizo lingine lolote ni KUONGEZA TATIZO HILO!.

Inasadikika pia maji haya yanatumika katika baadhi ya misiba, (yanatiwa katika vyakula vya misibani), na katika baadhi ya vyakula vya biashara, na matumizi mengine,

Ikiwa unahudhuria mazishi yoyote yale *(yawe ya kikristo au sio ya kikristo),* hakikisha unatakasa vyakula vyote kwa Imani kwa damu

ya YESU kabla ya kula!.. Usile tu!..Vile vile kila ununuacho kama bidhaa ya chakula, pasipo kujua asili ya utengenezaji wake, kabla ya matumizi, takasa kwa Imani kwa damu ya YESU.

Lakini si maji ya zamzam tu yenye shida kiroho, bali pia na maji yajulikanayo kama “ya upako yauzwayo katika baadhi ya makanisa”..yote yanabeba sifa moja na haya ya ZAMZAM.

Ukiona maji yanauzwa kwa kivuli cha upako, kwamba uyatumiapo utapata uponyaji au ufunguzi!, kuwa makini sana!.

Watumishi wa kweli wa Mungu, wanatumia maji kwa uongozo maalumu wa Roho Mtakatifu, na si kama utaratibu au mwenendo wa mara zote, kwamba kila tatizo ni maji na tena yanauzwa!, na tena yanaaminishwa kuwa ndio kitu kiponyacho!, hayo ni mafundisho ya ibilisi, ambayo ni muhimu kuwa nayo makini!.

Ukikuta maji yanauzwa usinunue!, ukikuta mafuta yanauzwa usinunue!..Ibilisi ni yule yule, anayefanya kazi kwenye kila kitu kilicho kinyume na Neno la Mungu.

Usikose Makala zijazo…

Je umempokea YESU kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako?..kumbuka yeye pekee ndiye Njia ya kufika mbinguni, na si mwanadamu yoyote aliye hai au aliyekufa.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

UKWELI KUHUSU UISLAMU Sehemu ya kwanza: (Msikiti wa AL-Aqsa).

HAJIRI NI KAMA MLIMA SINAI ULIOKO ARABUNI.

JE! NI CHEMCHEMI IPI INATOKA NDANI YAKO, YA MITO AU YA KISIMA?

JE KUNA UISLAMU KATIKA BIBLIA?

LAKINI NINYI, NDUGU, MSIKATE TAMAA KATIKA KUTENDA MEMA.

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp